JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

Ofisi ya Waziri Mkuu

Februari, 2004

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

*Ofisi ya Waziri Mkuu*

*Februari, 2004*

**YALIYOMO**


| | | |
|---|---|---|
| **1.0** | **UTANGULIZI** | **1** |
| **1.1** | **KABLA YA UHURU** | **1** |
| **1.2** | **BAADA YA UHURU NA AZIMIO LA ARUSHA** | **1** |
| **1.3** | **MADARAKA MIKOANI** | **1** |
| **1.4** | **UBINAFSISHAJI WA MASHIRIKA YA UMMA** | **2** |
| **1.5** | **TAFSIRI YA WANANCHI** | **3** |
| **2.0** | **HALI HALISI NA CHANGAMOTO** | **3** |
| **2.1** | **HALI HALISI** | **3** |
| **2.2** | **CHANGAMOTO** | **4** |
| **3.0** | **DIRA, MWELEKEO NA MADHUMUNI** | **4** |
| **3.1** | **DIRA** | **4** |
| **3.2** | **MWELEKEO** | **5** |
| **3.3** | **MADHUMUNI** | **6** |
| **4.0** | **SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI** | **7** |
| **4.1** | **KUKUZA UCHUMI NA KUJENGA MAZINGIRA YA UWEKEZAJI** | **7** |
| | 4.1.1. Hoja | 7 |
| | 4.1.2 Tamko la Sera | 7 |
| | 4.1.3 Mikakati | 7 |
| **4.2** | **MFUMO NA UTAWALA WA KODI, SHERIA, KANUNI, LESENI NA HUDUMA NYINGINE ZA SERIKALI** | **8** |
| | 4.2.1 Mfumo wa Kodi | 8 |
| | 4.2.1.1 Hoja | 8 |
| | 4.2.1.2 Tamko la Sera | 8 |
| | 4.2.1.3 Mikakati | 8 |
| | 4.2.2 Sheria, Kanuni na Taratibu | 9 |
| | 4.2.2.1 Hoja | 9 |
| | 4.2.2.2 Tamko la Sera | 9 |
| | 4.2.2.3 Mikakati | 9 |
| | 4.2.3 Leseni | 10 |
| | 4.2.3.1 Hoja | 10 |
| | 4.2.3.2 Tamko la Sera | 10 |
| | 4.2.3.3 Mikakati | 10 |
| | 4.2.4 Ufanisi wa Huduma zitolewazo na Serikali | 10 |
| | 4.2.4.1 Hoja | 10 |

4.2.4.2 Tamko la Sera 10
4.2.4.3 Mikakati 11
**4.3 MITAJI 11**
4.3.1 Hoja 11
4.3.2 Tamko la Sera 11
4.3.3 Mikakati 12
4.3.3.1 Kuimarisha na Kuboresha Vyanzo vya Akiba 12
4.3.3.2 Mikakati ya Kuwezesha Mabenki Yakopeshe 12
4.3.3.3 Mikakati ya Kuinua Hadhi ya Wananchi ili Wakopesheke 14
**4.4 KUINUA VIWANGO VYA UJUZI NA UZOEFU 15**
4.4.1 Hoja 15
4.4.2 Tamko la Sera 15
4.4.3 Mikakati 15
**4.5 MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI 16**
4.5.1 Hoja 16
4.5.2 Tamko la Sera 16
4.5.3 Mikakati 16
**4.6 UBINAFSISHAJI 18**
4.6.1 Hoja 18
4.6.2 Tamko la Sera 18
4.6.3 Mikakati 18
**4.7 MASOKO 19**
4.7.1 Hoja 19
4.7.2 Tamko la Sera 19
4.7.3 Mikakati 19
**4.8 USHIRIKA 20**
4.8.1 Hoja 21
4.8.2 Tamko la Sera 21
4.8.3 Mikakati 21
**4.9 ARDHI 21**
4.9.1 Hoja 21
4.9.2 Tamko la Sera 22
4.9.3 Mikakati 22
**5.0 MFUMO WA USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA SERA YA UWEZESHAJI 22**

## SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 KABLA YA UHURU

Kutokana na sababu za kihistoria, wananchi hawakushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi, kwa kuwa walinyimwa fursa. Hali hii ilikuwepo wakati wa ukoloni ambapo wananchi wengi waliwekewa vikwazo kushiriki katika uchumi ili watawalike kirahisi. Wananchi walilazimika kujishughulisha na uchumi wa sekta isiyo rasmi wakati sehemu kubwa ya sekta rasmi ilishikwa na watawala wa kikoloni na wageni. Wakoloni walitumia mbinu mahsusi kuwaendeleza wazungu na wananchi wachache. Mbinu hizo ni pamoja na utoaji wa mikopo, utoaji wa elimu, ugawaji wa ardhi na utoaji wa leseni za biashara. Baadhi ya mbinu hizo zinaweza kutumika hivi sasa kurekebisha hali hiyo na kuwawezesha wananchi kumiliki sehemu kubwa ya uchumi.

### 1.2 BAADA YA UHURU NA AZIMIO LA ARUSHA

Uhuru ulipopatikana mwaka wa 1961, Wananchi walipata madaraka ya kisiasa lakini sehemu kubwa ya uchumi bado ilibaki mikononi mwa wageni na baadhi ya Watanazania. Hali hiyo ilileta kero na ni mojawapo ya sababu muhimu ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha, mwaka wa 1967. Azimio hilo lilikuwa mkakati muhimu wa kuhakikisha kwamba wananchi kwa pamoja kupitia dola wanashika njia kuu za uchumi. Shughuli zote za uzalishaji na utoaji wa huduma ziliundiwa mashirika ya umma. Hata hivyo, mashirika ya umma mengi yaliendeshwa kwa hasara na yaliendesha shughuli za kiuchumi kwa kutumia mtaji na ruzuku kutoka Serikalini.

### 1.3 MADARAKA MIKOANI

(i) Kabla na baada ya Uhuru kuna vyombo ambavyo viliongeza chachu ya wananchi kushiriki katika shughuli za uchumi. Kwanza ni Vyama vya Ushirika hasa katika uzalishaji, utoaji mikopo ya pembejeo, huduma za ugani na masoko ya mazao kadhaa kama vile pamba na kahawa. Pili, ni Serikali za Mitaa ambazo zilikuwa na uwezo wa kuwashirikisha kwa karibu wananchi katika shughuli za uchumi. Aidha, katika mwaka

1973 Serikali ilianzisha Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) kwa ajili ya kuendeleza viwanda vidogo nchini.

(ii) Kutokana na matatizo mbalimbali, mwaka 1972, Serikali za Mitaa zilivunjwa na badala yake ukawekwa mfumo wa Madaraka Mikoani uliotegemea zaidi Serikali Kuu kuliko nguvu za wananchi. Vile vile, vyama vya ushirika vilivunjwa mwaka 1976 na badala yake ulianzishwa mfumo wa Washirika kama Jumuiya ya Chama ambayo iliendeshwa kiserikali. Kwa maana hiyo ile chachu ya kuongeza nguvu za wananchi wenyewe kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi ilipungua kwa kiasi kikubwa. Hatua zilizochukuliwa na Serikali mwaka wa 1982 kuunda upya Serikali za Mitaa na kurudisha Vyama vya Ushirika mikononi mwa wananchi mwaka wa 1984 ni sehemu ya kutambua makosa yaliyofanyika hapo awali ya kuweka miundo ambayo iliendeshwa na nguvu ya Serikali kuliko ya wananchi wenyewe. Kwa hiyo Sera ya Uwezeshaji inazingatia kuwepo kwa Vyama vya Ushirika na Serikali za Mitaa kwa lengo la kuhakikisha kwamba kwa kiasi kikubwa vinaendeshwa kwa kuwapa wananchi madaraka ya kuamua na kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi.

(iii) Mchango wa SIDO katika kuendeleza viwanda vidogo vinavyoendeshwa na wananchi umekuwa mkubwa kwa kutumia mbinu za mafunzo, ushauri na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu. Hata hivyo, mafanikio yake yangekuwa makubwa zaidi kama shughuli za SIDO zingekuwa zimetekelezwa chini ya mwongozo wa Sera ya Uwezeshaji. SIDO haikuweza kutekeleza wajibu wake kikamilifu kutokana na kutokupata fedha za kutosha kuendeshea shughuli zake. Aidha, SIDO ilichelewa kujiweka sawa kuendesha shughuli zake katika mazingira mapya ya ushindani. Hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali kuiongezea SIDO uwezo na ambazo SIDO imechukua kubadilisha muundo wake na kujiweka sawa ili kuhimili ushindani zinaendana na maudhui ya Sera ya Uwezeshaji.

## 1.4 UBINAFSISHAJI WA MASHIRIKA YA UMMA

Mwaka wa 1992, Sera ya Ubinafsishaji ilianzishwa baada ya kuona kwamba mashirika ya umma yalikuwa mzigo kwa Serikali ambayo haikuwa na fedha

za kuyaendesha na kuyaendeleza hata kufikia uamuzi wa kuyarekebisha na mengine kuyabinafsisha. Katika ubinafsishaji huo, sehemu kubwa ya wananchi hawakushiriki ipasavyo katika zoezi hilo kwa kuwa hawakuwa na elimu ya biashara, ujuzi na mitaji. Aidha, utaratibu wa kuanzisha Amana ya Ubinafsishaji (Privitezation Trust) kwa ajili ya kusaidia wananchi kushiriki kununua hisa katika mashirika ya umma yaliyokuwa yamebinafsishwa haukutekelezwa, sababu mojawapo ikiwa, ni kutokuwepo kwa Sera ya Uwezeshaji. Serikali kwa kuzingatia yote haya,imeamua kuwe na Sera ya Uwezeshaji ambayo itakuwa mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wa wananchi katika sekta zote.

## 1.5 TAFSIRI YA WANANCHI

Walengwa wa Sera ya Uwezeshaji ni wananchi. Makampuni ya wananchi ni yale ambayo yamesajiliwa Tanzania ambayo walengwa wanamiliki asilimia isiyopungua hamsini ya hisa zote za makampuni hayo. Sera ya Uwezeshaji itajumuisha wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyakazi na wafanya biashara katika sekta mbalimbali na makundi mengine. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji inatoa mwongozo utakaotumika kutafsiri uwezeshaji utakavyokuwa katika sehemu mbalimbali kulingana na mazingira ya sekta husika. Mikakati itakayobuniwa na sekta mbalimbali, itafafanua uwezeshaji utakuwaje katika shughuli moja moja. Kwa mantiki hiyo, ni wajibu wa kila sekta kufafanua na kuchanganua jinsi ya kutekeleza Sera hii kulingana na majukumu yake.

# 2.0 HALI HALISI NA CHANGAMOTO

## 2.1 HALI HALISI

Ushiriki wa wananchi wengi katika shughuli za uchumi wa kisasa ni duni. Sehemu kubwa ya uchumi huo imeshikwa na wageni au Watanzania wachache kwa maana ya Sera hii. Hali hiyo inapingana na dhana ya kuleta maendeleo yanayonufaisha na kutoa nafasi ya maendeleo kwa wananchi wengi. Kisiasa hali ya kutokuwa na fursa ya kushiriki kikamilifu katika uchumi imesababisha malalamiko miongoni mwa wananchi. Wengi wao wameshindwa kushiriki kwa sababu ya uwezo mdogo kimtaji, ukosefu wa ujuzi na uzoefu wa biashara pamoja na matatizo yanayohusiana na kutokukopesheka. Aidha, hali hiyo imechangiwa na kutokuwa na Sera madhubuti ya kukabili tatizo la uwezeshaji.

## 2.2 CHANGAMOTO

Katika kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za uchumi, wananchi wanakabiliwa na vikwazo vifuatavyo:-

(i) Upatikanaji wa mitaji.

(ii) Ukosefu wa ujuzi na uzoefu vikichochewa na upungufu katika elimu, mafunzo, mila na desturi potofu na mtazamo wa kimaendeleo.

(iii) Matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sera ya ubinafsishaji na mfumo wake.

(iv) Ukosefu wa masoko ya uhakika au uwezo wa kuingia katika masoko yenye ushindani.

(v) Ukosefu wa ushirikiano, ushirika hafifu na ukosefu wa sauti ya pamoja ya makundi mbalimbali ya wananchi katika kusimamia maslahi yao na kukabili matatizo yanayowakwaza wasishiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi ndani ya sekta zao.

(vi) Aidha, vikwazo vingine vya ujumla vinavyoathiri ushiriki katika uchumi ni:-

a) Udhaifu wa mfumo wa kodi, sheria, kanuni na leseni pamoja na huduma nyingine za Serikali.

b) Upungufu wa miundombinu ya kiuchumi, kijamii na kiutawala.

Sera ya Uwezeshaji inalenga kuondoa vikwazo hivi ili kutoa nafasi nzuri zaidi kwa makundi mbalimbali kushiriki kikamilifu zaidi katika shughuli za uchumi.

# 3.0 DIRA, MWELEKEO NA MADHUMUNI

## 3.1 DIRA

Uwezeshaji wa wananchi kushiriki kikamilifu ktika shughuli za uchumi ni sehemu ya Dira ya maendeleo ya Taifa kufikia mwaka 2025. Kufikia wakati huo, sehemu kubwa ya uchumi wa Tanzania inatarajiwa kumilikiwa na Watanzania

wenyewe. maendeleo hayo yatajumuisha Watanzania wote pamoja na kutoa nafasi kwa makundi yote kujiendeleza kikamilifu hasa yale makundi yenye uwezo mdogo. Pamoja na kuwapa nafasi zaidi wanyonge, yatawekwa mazingira mazuri ya ujenzi wa uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani katika soko la dunia katika mazingira ya utandawazi.

## 3.2 MWELEKEO

(i) Mwelekeo wa Sera ya uwezeshaji utazingatia Sera ya kuendeleza na kuipa nafasi kubwa zaidi sekta binafsi pamoja na kuzingatia masharti ya kuendesha uchumi katika mazingira ya nguvu ya soko. Kwa maana hiyo, mbinu na mikakati itakayotumika katika kuwawezesha wananchi kiuchumi itatambua mchango wa sekta isiyo rasmi na kuchukua hatua za kuiboresha.

(ii) Sera ya Uwezeshaji italenga katika maeneo yenye kuleta matokeo ya haraka hasa yale yanayogusa maisha ya wananchi wenye ujasiriamali katika kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu, ujenzi, biashara, utalii, madini, viwanda, na usafirishaji. Aidha, Sera itaweka mikakati ya makusudi kuwawezesha walengwa walioko tayari katika sekta hizo kufanya vizuri zaidi katika maeneo yao. Maeneo ambayo yanafaa kuachiwa walengwa peke yao na yale yatakayofanywa kwa ubia na wageni yataainishwa.

(iii) Sera ya uwezeshaji wa Wananchi itawezesha kujenga uwezo wa ushindani katika soko la ndani ambalo bidhaa za nje zinaingia, soko la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, SADC, Jumuiya nyingine na soko la dunia. Vile vile, Sera ya Uwezeshaji itainua ubora wa bidhaa zinazozalishwa, kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza ujuzi unaotumika kuzalisha mali. Pale ambapo miradi mikubwa ya wawekezaji itaanzishwa, miradi hiyo itatoa fursa za kuzishirikisha shughuli za wananchi. Sera ya Uwezeshaji itatekelezwa kwa kuwashirikisha wadau husika pamoja na Serikali yenyewe. Kwa hiyo, jukumu la utekelezaji wa Sera hii si la Serikali peke yake bali linajumuisha sekta binafsi pamoja na wadau wengine. Aidha, utekelezaji utategemea sana utawala bora na utoaji wa huduma za jamii kwa ufanisi mkubwa pamoja na kuwa na mtazamo na fikra sahihi kuhusu uwezeshaji.

## 3.3 MADHUMUNI

Madhumuni ya Sera hii ni kutoa mwongozo wa jumla utakaohakikisha kwamba, wananchi wanapata fursa za kiuchumi katika sekta mbalimbali. Kwa maana hiyo, Sera za kisekta zitalenga katika kuwainua wananchi kwa kuwapendelea zaidi ikibidi na kuwawezesha kuwa na kauli na ushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kwa mantiki hiyo, Sera ya Uwezeshaji inajielekeza katika:-

(i) Kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi.

(ii) Kuboresha mfumo na utawala wa kodi.

(iii) Kurekebisha sheria, kanuni na taratibu mara kwa mara ili ziendane na dhana ya uchumi unaoendeshwa kwa nguvu za soko.

(iv) Kuboresha na kurahisisha utoaji wa leseni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

(v) Kuboresha ufanisi wa huduma zitolewazo na Serikali.

(vi) Kurahisisha upatikanaji wa mitaji na kuwezesha wananchi kukopesheka.

(vii) Kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu.

(viii) Kuimarisha miundombinu na kuwashirikisha wananchi katika shughuli za miundombinu.

(ix) Kuboresha mazingira yatakayowezesha wananchi kushiriki kikamilifu zaidi katika ubinafsishaji wa mashirika ya umma.

(x) Kuimarisha uwezo wa kuzalisha bidhaa bora, kutoa huduma kwa ufanisi, usanifu na ustadi wa kiwango cha juu na kutoa huduma za kutafuta masoko na kutumia manunuzi ya Serikali kuwasaidia wananchi kupata masoko.

(xi) Kuhimiza na kuimarisha maendeleo ya ushirika.

(xii) Kutumia ardhi kama chombo cha kuweka chachu ya uwezeshaji.

(xiii) Kuweka mfumo thabiti wa usimamizi wa Sera ya Uwezeshaji.

## 4.0 SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

## 4.1 KUKUZA UCHUMI NA KUJENGA MAZINGIRA YA UWEKEZAJI

### 4.1.1. Hoja

Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Tanzania ni kidogo na mazingira ya uwekezaji ambayo ndiyo chachu ya ukuaji wa uchumi endelevu ni hafifu.

### 4.1.2 Tamko la Sera

Jitihada za kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi nchini ni muhimu ziendane na ukuaji wa uchumi unaojumuisha na kunufaisha Watanzania wengi, kuongeza vipato vyao pamoja na kuinua hali zao za maisha.

Sera ya Uwezeshaji inaweka mazingira bora yatakayochochea uwekezaji na uzalishaji kwa ajili ya masoko ya ndani, ya kanda za Afrika na ya dunia.

### 4.1.3 Mikakati

Ili kukuza uchumi madhubuti na kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji, mikakati ifuatayo itatekelezwa:-

(i) Kuzielekeza Sera za kisekta katika kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi.

(ii) Kuhakikisha kwamba hali ya amani na utulivu inadumishwa.

(iii) Kuhakikisha kuwa Sera za kiuchumi zinatabirika na mfumuko wa bei unadhibitiwa.

(iv) Kuboresha miundombinu ili wananchi waweze kuitumia kwa gharama nafuu.

(v) Kuwezesha kuingia ubia na kuboresha mitandao kati ya wananchi walio wengi na wawekezaji waliobobea ili kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika na nguvu za wenye uwezo.

(vi) Kuweka na kutekeleza Sera na mikakati madhubuti ya kuendeleza mauzo katika masoko ya Kanda ya Afrika na masoko ya dunia. Hii ni pamoja na kuharakisha utekelezaji wa Maeneo Maalum ya Mauzo ya Nje na Maeneo Maalum ya Kiuchumi na Kituo cha Uendelezaji wa Masoko. Kujenga uwezo wa wananchi ili waweze kumudu uwekezaji katika mazingira ya soko huria na ushindani na kuvutia wawekezaji kuingia nao ubia.

(vii) Kuzalisha bidhaa bora kwa gharama za chini au zinazolingana na za ushindani.

(viii) Kuhimiza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

(ix) Kuunda kamati za uwezeshaji zinazojumuisha wadau katika ngazi mbalimbali.

## 4.2 MFUMO NA UTAWALA WA KODI, SHERIA, KANUNI, LESENI NA HUDUMA NYINGINE ZA SERIKALI

### 4.2.1 Mfumo wa Kodi

#### 4.2.1.1 Hoja

Pamoja na juhudi zinazoendelea za kuboresha mfumo wa kodi, bado mfumo na utawala wa kodi uliopo hautoi fursa inayowezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi.

#### 4.2.1.2 Tamko la Sera

Kuboresha mfumo na utawala wa kodi ili kuhamasisha uwekezaji.

#### 4.2.1.3 Mikakati

Mfumo na utawala wa kodi utaboreshwa kwa kuchukua hatua za utekelezaji zifuatazo:-

(i) Utaratibu wa kuwapa wawekezaji wakubwa unafuu wa kodi utapanuliwa kuwahusisha pia wananchi ili nao wapate unafuu huo kama wawekezaji wengine.

(ii) Kuendelea kushirikisha wadau mbalimbali ili kuboresha mfumo na utawala wa kodi mara kwa mara.

(iii) Kodi ya kuendeleza ujuzi ya asilimia sita inayochangiwa na waajiri, itatumika kuendeleza ujuzi kwa kiwango kikubwa zaidi.

(iv) Serikali itatoa unafuu wa kodi kama mchango wa Serikali katika kugharamia mafunzo yanayotolewa na waajiri kwa wafanyakazi wao.

(v) Serikali itatoa elimu kuhusu sheria ya kodi, viwango na aina mbalimbali za kodi kwa wananchi ili wajue wazi kiasi cha kodi wanachostahili kulipa.

(vi) Serikali itaendelea kuhuisha kodi zinazotozwa na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa lengo la kuondoa kero na kuvutia uwekezaji.

### 4.2.2 Sheria, Kanuni na Taratibu

#### 4.2.2.1 Hoja

Baadhi ya sheria, kanuni na taratibu zilizopo haziendani na dhana ya uchumi wa uwezeshaji

#### 4.2.2.2 Tamko la Sera

Kurekebisha sheria, kanuni na taratibu zilizopitwa na wakati ili ziendane na Sera ya Uwezeshaji**.**

#### 4.2.2.3 Mikakati

Mikakati itakayotumika kurekebisha sheria, kanuni na taratibu ili ziendane na Sera ya Uwezeshaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutunga Sheria ya Uwezeshaji na kurekebisha sheria nyingine ili ziwe na mwelekeo wa kuwawezesha wananchi kiuchumi.

(ii) Sheria ya Uwezeshaji itaunda vyombo vitakavyosimamia uwezeshaji.

### 4.2.3 Leseni

#### 4.2.3.1 Hoja

Utoaji wa leseni unaathiriwa na wingi, urasimu na ukiukwaji wa sheria za leseni.

#### 4.2.3.2 Tamko la Sera

Leseni za biashara zitatumika kama njia ya kuratibu shughuli za uchumi na sio tu kama chanzo cha mapato ya Serikali.

#### 4.2.3.3 Mikakati

Ili kupunguza wingi wa leseni, urasimu katika kutoa leseni, gharama kubwa na ukiukwaji wa sheria za leseni mikakati ifuatayo itatekelezwa:-

(i) Elimu itatolewa kwa Halmashauri na Mamlaka za utoaji leseni ili leseni zitolewe kwa kufuata sheria inayohusika.

(ii) Sheria ndogo za Halmashauri zinazopingana na sheria ya leseni zitarekebishwa.

(iii) Leseni zitatolewa kwa kufuata sheria inayohusika na leseni hiyo na hazitahusisha masuala mengine yaliyo nje ya sheria husika.

(iv) Leseni mbalimbali zitaainishwa ili kuona uwezekano wa kuwa na kituo kimoja katika kila mamlaka na katika ngazi za vijiji hadi Taifa.

### 4.2.4 Ufanisi wa Huduma zitolewazo na Serikali

#### 4.2.4.1 Hoja

Upo udhaifu katika utoaji wa huduma mbalimbali zitolewazo na Serikali kwa wananchi.

#### 4.2.4.2 Tamko la Sera

Serikali itaimarisha ufanisi wa utoaji wa huduma kwa umma hasa katika kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Aidha, watumishi watawezeshwa kuwa na mtazamo na fikra sahihi katika

kutoa huduma za hali ya juu zitakazowezesha kusimamia vema uchumi katika mazingira ya utandawazi.

#### 4.2.4.3 Mikakati

Serikali itaboresha mazingira ya kazi ya Watumishi wake kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo ya hali ya juu na vitendea kazi bora.

(ii) Kuboresha maslahi ya watumishi ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kuwekeza.

(iii) Kufanya utafiti wa namna ya kuwawezesha watumishi kutumia pensheni zao katika kuwekeza kabla hawajastaafu.

## 4.3 MITAJI

### 4.3.1 Hoja

Upatikanaji wa mitaji kwa wananchi ni mgumu kwa sababu ya:

(i) Ufinyu wa vyanzo vya akiba kutokana na kipato kidogo na kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba.

(ii) Kuwepo kwa vizuizi vinavyosababisha mabenki kusita kutoa mikopo. Kwa mfano: gharama kubwa za kuhudumia utoaji wa mikopo ambazo zinasababishwa na ukosefu wa vitambulisho vya Taifa, na kutokuwa na utaratibu mzuri wa kupata habari za waomba mikopo.

(iii) Udhaifu unaowafanya wasikopesheke, kama vile ukosefu wa ujuzi wa kuandaa na kusimamia miradi inayokopesheka, ukosefu wa dhamana na mtaji wa kuchangia uanzishaji wa miradi.

### 4.3.2 Tamko la Sera

Serikali itaweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mitaji kwa kuimarisha na kuboresha vyanzo vya akiba, itachukua hatua za kuondoa vikwazo mbalimbali ili kuwezesha mabenki kukopesha kikamilifu amana zilizopo na kwa gharama nafuu, na itaweka mikakati ambayo utekelezaji wake utainua hali na hadhi ya wananchi ili wakopesheke.

### 4.3.3 Mikakati

#### 4.3.3.1 Kuimarisha na Kuboresha Vyanzo vya Akiba

Serikali itachukua hatua madhubuti katika maeneo manne ili kuimarisha vyanzo vya akiba na mitaji kwa wananchi:

(i) Itawahimiza wananchi kuanzisha uwekezaji wa pamoja ili wajipatie mitaji ya kuanzishia shughuli zao za kiuchumi

(ii) Kwa kushirikiana na vyama mbalimbali vya walengwa na Chama cha Taasisi Ndogo Ndogo za fedha, itawahamasisha wananchi katika sekta mbalimbali kujiunga na taasisi ndogo ndogo za fedha ili waweze kupata sehemu za kuwekeza akiba zao kwa pamoja, hivyo kujenga mitaji ambayo baadaye itakuwa chimbuko la kuwakopesha wanachama wake. Ni rahisi kwa taasisi hizi kukopesha wanachama wake kwa vile zinawafahamu vizuri na ziko karibu na shughuli zao. Vyama hivi pia vinaweza kuwa wakala kwa mabenki makubwa katika kutoa mikopo, na kwa maana hiyo kuyapunguzia gharama za kutafuta habari muhimu za kuwezesha mabenki kumfahamu vizuri mkopaji mmoja mmoja, kitendo ambacho husababisha kuongezeka kwa gharama za mabenki na kuchangia kupanda kwa riba au kufanya wananchi wasikopesheke.

(iii) Itafanya utafiti wa kina ili kuainisha mbinu na taratibu nzuri zitakazowawezesha wanachama wa pensheni kutumia sehemu ya pensheni zao kwa ajili ya kuongeza uwezo wao wa kukopa kwa minajili ya kuanzisha miradi ya kiuchumi au kununulia hisa katika makampuni mbalimbali.

(iv) Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zitabuni mbinu za kujijengea mitaji ya kuimarisha miundombinu itakayochochea maendeleo ya wawekezaji katika sehemu mbalimbali nchini. Njia mojawapo ni kutoa *"bonds"* za muda mrefu kupitia soko la mitaji ili kupata fedha za kuanzisha mifuko mbalimbali ya kuwasaidia wananchi au kuwekeza katika miundombinu muhimu.

#### 4.3.3.2 Mikakati ya Kuwezesha Mabenki Yakopeshe

Hali halisi inaonyesha kwamba ni asilimia 30 – 40 tu ya amana zote zilizowekezwa katika mabenki nchini zimetolewa kama mikopo. Aidha, taasisi za fedha za kimataifa zina fedha ambazo zinaweza kukopwa endapo miradi inayokubalika itakuwepo. Ili kuyawezesha mabenki kukopesha zaidi, Serikali itatumia mikakati ifuatayo:

(i) Kupitia Benki Kuu na mabenki ya biashara, chombo cha kuweka kumbukumbu za wakopaji kitaanzishwa kwa nia ya kuyarahisishia mabenki kutambua wananchi walio na tabia ya kukopa na kulipa madeni. Kwa maana hiyo, gharama ya kutafuta habari kamili za wakopaji zitapungua na hivyo viwango vya riba vinaweza kupungua pia.

(ii) Itaunda Mfuko Maalum utakaosimamiwa na taasisi ya kutoa dhamana ya kuwawezesha wananchi kupata mikopo kutoka katika mabenki kwa ajili ya miradi ya kati na mikubwa, au kutoa mitaji kwa wananchi watakaoonzisha makampuni ya ubia na wawekezaji wa nje. Mfuko huo utajenga uwezo wa kutathmini miradi na kusimamia utekelezaji wake.

(iii) Itafanya utafiti ili kubuni vivutio ambayo vitashawishi mabenki kuanzisha vitengo vya mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya kukopesha miradi ya maendeleo.

(iv) Serikali itafanya tathmini ya mifuko mbalimbali ambayo hutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi ili kupata mbinu mpya za kuiboresha, ikiwa ni pamoja na kutumia mabenki yaliyopo kuendesha mifuko hiyo. Aidha, Serikali itaanzisha mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi utakaosimamiwa na mabenki kwa ajili ya kutoa mikopo ya gharama nafuu, kwa masharti ambayo Serikali itakubaliana na mabenki hayo. Katika sekta ya kilimo, Serikali itaanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wanaotaka kuwekeza na kutoa mikopo kwa wakulima na wafugaji.

(v) Itaanzisha utaratibu wa kutoa vitambulisho kwa raia wote nchini kwa nia ya kusaidia kupunguza gharama za mabenki kutafuta taarifa muhimu za wakopaji.

(vi) Itahakikisha kwamba kanuni zinazotawala utekelezaji wa Sheria za Ardhi za mwaka wa 1999 zinafuatwa ili kuwezesha hati miliki ya ardhi kutumika kama dhamana ya kuombea mikopo. Aidha, Mahakama ya Ardhi itaimarishwa ili kushughulikia kwa wepesi zaidi kesi za ardhi ambazo kucheleweshwa kwake huwa kikwazo kwa mabenki kutoa mikopo.

(vii) Itaongoza kasi ya upimaji viwanja mijini na vijijini, na itaboresha taratibu za utoaji hati miliki ili ardhi iweze kutumika kama chombo cha uwezeshaji.

(viii) Kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Taasisi za kutoa mikopo midogo midogo mwezi Februari 2003, Serikali itahakikisha sheria hii inatekelezwa haraka. Taasisi zitakazoandikishwa chini ya sheria hii zitaweka utaratibu wa kuwakopesha wananchi mikopo midogo midogo kwa masharti nafuu.

### 4.3.3.3 Mikakati ya Kuinua Hadhi ya Wananchi ili Wakopesheke

Wananchi wengi hawakopesheki kwa sababu hawana uzoefu na ujuzi wa kutosha kutayarisha miradi na kuiendesha hadi iweze kupata faida na kujenga uwezo wa kulipa madeni. Aidha, mabenki husita kutoa mikopo hata kwa miradi iliyosanifiwa vizuri kutokana na wananchi kutokuwa na uhakika wa masoko kwa bidhaa zitakazozalishwa na miradi, au kwa kutofikia viwango vya ubora au wingi unaohitajika ili kupata masoko ya nje. Serikali itawasaidia wananchi kuondokana na tatizo hili kwa njia zifuatazo:

(i) Itasaidia kuboresha huduma za usanifu wa miradi zinazotolewa na taasisi zake na makampuni ya wananchi ya wataalam waelekezi. Aidha, itachangia gharama ambazo wananchi watatakiwa kulipa ili waandikiwe miradi ambayo inaweza kukopesheka.

(ii) Halmashauri za Wilaya na Miji zitaanzisha vitengo kwa ajili ya kubuni na kusanifu miradi ya wananchi katika maeneo yao.

(iii) Taasisi za elimu ya juu zitawezeshwa kutoa mafunzo ya kuinua viwango vya ujuzi wa kubuni na kuendesha miradi. Aidha, Serikali itatoa mafunzo maalum kwa wananchi yatakayowawezesha kupata ujuzi wa kuanzisha, kusimamia, na kuendesha miradi katika vyuo vitakavyoteuliwa hapa nchini.

(iv) Kwa kuwa wananchi wengi hawakopesheki kwa vile hawafahamiki na mabenki, japo wanafahamika vizuri na vyama vyao vya biashara, Serikali itaimarisha vyama hivi ili wananchi waweze kutumia umoja huo kuwatolea dhamana ili waweze kukopesheka.

(v) Itazishauri taasisi za sekta binafsi zianze kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuingia ubia na wawekezaji kutoka nje ya nchi ili kutumia uzoefu wao wa kiufundi, menejimenti na masoko waliyonayo katika kushawishi mabenki kutoa mikopo kwa miradi yao. Pia taasisi hizo zitatakiwa kusaidia kuwatayarisha wanachama wao kujenga

tabia ya kulipa mikopo na kushirikiana na mabenki kuhakiki kama wanaoomba mikopo wanakopesheka.

## 4.4 KUINUA VIWANGO VYA UJUZI NA UZOEFU

### 4.4.1 Hoja

Wananchi wanashindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi kwa vile wanakabiliwa na vikwazo vinavyotokana na elimu ndogo pamoja na ujuzi na uwezo mdogo. Kiwango kidogo cha elimu kinachangia baadhi ya wananchi kuendeleza mila na desturi potofu zisizo na upeo wa maendeleo. Aidha, mfumo wa elimu haujengi fursa ya uendelezaji wa ujasiriamali.

### 4.4.2 Tamko la Sera

Serikali itaangalia upya mfumo wa elimu kwa nia ya kuongeza kina cha mtazamo wa kisayansi ili kukabili mila na desturi potofu zinazodumaza maendeleo, na kumjenga mwananchi anayejiamini, mbunifu na mwenye ari ya kuzalisha na kufanya biashara ama shughuli zingine kwa makini na ustadi mkubwa. Kwa maana nyingine, mfumo wetu wa elimu utatakiwa kuwajengea wananchi misingi ya ujasiriamali. Mfumo wa mafunzo utahakikisha kwamba ujuzi unaongezeka wakati wote kulingana na mahitaji ya ushindani katika masoko mbalimbali.

### 4.4.3 Mikakati

Ili kutekeleza Sera ya kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu wa wananchi;

(i) Serikali itahakikisha kwamba wananchi wanasaidiwa kuongeza ujuzi, kupata uzoefu pamoja na kuwawezesha kuhimili ushindani katika Masoko ya ndani na nje ya nchi.

(ii) Serikali itaanzisha utaratibu wa kuweka vishawishi kwa kampuni na vyuo vya watu binafsi kuanzisha mafunzo maalum kwa kutumia fedha itokanayo na kodi ya kuendeleza ujuzi ili kusaidia uendelezaji wa vyuo hivyo.

(iii) Serikali itasaidia vyuo au kampuni mbalimbali kuchangia gharama za mafunzo ili kuhamasisha wananchi kujiendeleza kiufundi na kiujuzi katika vyuo vitakavyokuwa vinakidhi mahitaji yao. Utaratibu huu

utasaidia kuendeleza vyuo vilivyopo na kuhamasisha uanzishaji wa mafunzo yanayoendana na utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji. Pale ambapo itabidi utaalamu utoke nje au watalaam wa ndani kwenda nje, utaratibu huu wa kuchangia gharama za mafunzo utatumika ili kuhamasisha wananchi kujiendeleza zaidi kiufundi na kiteknolojia.

(iv) Mitaala ya shule itarekebishwa ili kutoa elimu na ujuzi wa ujasiriamali ikiwa ni pamoja na kumwezesha mhitimu kujiamini, kuwa mbunifu na kuwa na ari ya kufanya kazi kwa makini na ustadi mkubwa.

(v) Serikali itaanzisha taasisi ambayo itasimamia masuala yote ya kuwawezesha wananchi kwa njia ya kuwaongezea ujuzi. Taasisi hii ya ujasiriamali itaandaa mitaala ambayo vyuo mbalimbali nchini vitaitumia kuwaelimisha wananchi.

## 4.5 MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI

### 4.5.1 Hoja

Miundombinu ya kiuchumi iliyopo kama vile barabara, nishati na mtandao wa mawasiliano haitoshelezi katika kuwafikia wananchi kwa urahisi na kwa gharama zinazowiana na zile za washindani katika nchi jirani na nchi nyingine. Aidha, wananchi hawajashirikishwa kikamilifu katika kujenga, kutengeneza na kutoa huduma mbalimbali za uendeshaji wa miundombinu hiyo. Hali hiyo inawanyima wananchi fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi kupitia sekta ya miundombinu.

### 4.5.2 Tamko la Sera

Serikali itatenga fedha za kuboresha miundombinu. Aidha, itaweka mazingira mazuri ya kuhamasisha sekta binafsi katika kuwekeza na kuendeleza miundombinu.

### 4.5.3 Mikakati

Katika kuboresha miundombinu ili irahisishe harakati za kukuza uchumi na pia kuwawezesha wananchi, mikakati ifuatayo itatumika kulingana na aina ya miundombinu:-

(i) Serikali itahimiza mafunzo katika ngazi ya utawala ili kuweza kujenga uwezo wa kusimamia miradi mbalimbali ya miundombinu.

(ii) Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa makandarasi wananchi na watendaji wao.

(iii) Utaratibu utaandaliwa ili kuhakikisha kwamba makandarasi wananchi na kampuni zingine za wananchi ambazo zitashiriki katika kuboresha miundombinu zinapewa upendeleo maalum kama njia mojawapo ya kuwaendeleza wananchi.

(iv) Makandarasi wa nje watapewa kipaumbele pale watakapokuwa tayari kushirikiana na makandarasi wa ndani (walengwa) kwa ubia au kwa utaratibu wa '*subcontracting*'. Aidha, kazi zinazohitaji ujuzi na uzoefu ambazo haumo nchini zitafanywa na makandarasi wa nje na zile ambazo ziko chini ya uwezo wa hapa nchini zitatolewa kwa wananchi.

(v) Makampuni ya wananchi yatawezeshwa kupata mikopo kwa ajili ya kununulia vifaa vya ujenzi pale inapostahili. Mazingira mazuri yatawekwa ili watu binafsi wakiwemo wananchi waweze kuanzisha kampuni za kukodisha vifaa vya ujenzi wa miundombinu.

(vi) Serikali itahamasisha uundwaji wa bodi za utekelezaji wa shughuli za miundombinu zitakazohusisha wadau wa sekta husika pamoja na ushiriki au uwakilishi wa wananchi katika ngazi husika.

(vii) Serikali itashirikiana na wananchi binafsi au jumuiya zao kuweka utaratibu wa kuchangia katika kuimarisha ubora wa miundombinu.

### Barabara

(i) Tathmini itafanywa ili kujua maeneo ya kipaumbele katika ujenzi na uimarishaji wa barabara katika ngazi husika. Aidha, katika ngazi zote hizo uwezekano wa kushirikishwa kwa Serikali, sekta binafsi na wananchi wenyewe kutumia teknolojia ya nguvu kazi utafanyiwa tathmini kulingana na hali halisi.

### Mtandao wa Mawasiliano

(i) Tathmini itafanywa kubaini kiini cha gharama za simu kuwa juu kuliko zile za baadhi ya nchi jirani. Matokeo ya utafiti huo yatatumika kuandaa

mikakati ya kupunguza gharama za utumiaji wa simu kulingana na zile zinazotumika katika nchi jirani au nchi nyingine ambazo zinashindana na Tanzania.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itawezesha uboreshaji wa mitandao wa simu na "internet" mpaka vijijini ili kuviwezesha vijiji kuwasiliana kwa urahisi. Pale ambapo hakuna umeme, uwezekano wa kutumia teknolojia ya SIWAYA kueneza simu vijijini utazingatiwa. Vituo vya mawasiliano vitaanzishwa wilayani na vijijini kwa kuhamasisha sekta binafsi na wadau wengine.

**Huduma za Umeme**

(i) Serikali itaweka mikakati ya kupunguza gharama za umeme ili kupunguza gharama za uzalishaji.

(ii) Serikali itahamasisha uendelezaji wa njia za kuzalisha nishati mbadala na matumizi yake. Mkazo utawekwa katika kuendeleza nishati zinazotumia maliasili iliyoko nchini kama makaa ya mawe, mionzi ya jua, upepo.

(iii) Serikali itaweka mkazo katika kusambaza umeme vijijini kwa kuanzisha mfuko maalum. Mfuko huo utatumika pia kuendeleza vyanzo vingine vya nishati pale ambapo inafaa.

## 4.6 UBINAFSISHAJI

### 4.6.1 Hoja

Wananchi hawajashirikishwa kikamilifu katika ubinafsishaji.

### 4.6.2 Tamko la Sera

Serikali itabuni mbinu mbalimbali za kuwasaidia wananchi kumiliki mali au kununua hisa kwenye mashirika ya umma.

### 4.6.3 Mikakati

Serikali itatekeleza mikakati itakayohakikisha kwamba wananchi wanawezeshwa kununua hisa kwenye mashirika yatakayobinafsishwa. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuandaa utaratibu wa kuwawezesha wananchi kununua hisa kwenye mashirika ya umma.

(ii) Kuandaa utaratibu utakaohakikisha kwamba wananchi wanakopeshwa mitaji ya kununulia hisa au kuzishikilia hisa hadi hapo watakapokuwa na uwezo wa kuzinunua.

(iii) Kutafuta wataalam kutoka nje watakaoendesha kampuni kubwa, pale ambapo uzoefu utakuwa haupo nchini. Wataalam hao watafanya kazi kwa muda wakati wananchi wanaandaliwa kuchukua nafasi zao.

## 4.7 MASOKO

### 4.7.1 Hoja

Kwa ujumla masoko yote ya ndani na ya nje sasa yanakabiliwa na ushindani mkali kutokana na utandawazi. Mara nyingi bidhaa zinazozalishwa nchini hukosa masoko kutokana na uchache wa bidhaa zinazozalishwa na ubora kutofikia viwango vinavyokubalika kimataifa. Sababu nyingine ni gharama za uzalishaji mazao na bidhaa kuwa juu pamoja na ufungashaji usiokidhi viwango hivyo kushindwa kupata soko, ukosefu wa taarifa za masoko, kutokuendeleza masoko ya ndani ya nchi na kutotafuta masoko mapya nje ya yale tuliyoyazoea. Aidha, nchi zilizoendelea hutoa ruzuku kwa mazao yanayozalishwa na kuweka vikwazo vya kuzuia mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini kuingia kwenye masoko yao na hivyo kufanya ushindani usiwe wa haki.

### 4.7.2 Tamko la Sera

Serikali itahakikisha kwamba taarifa kuhusu mwenendo wa masoko zinapatikana kwa wazalishaji na itaendeleza masoko ya ndani, nchi jirani na ya soko la dunia. Aidha, wananchi watahimizwa kuzalisha mazao na bidhaa kulingana na matakwa ya soko. Vilevile Serikali itajikinga na madhara ya "dumping" ya bidhaa kutoka nje na itahakikisha kwamba wananchi wananufaika na soko linalotokana na manunuzi ya Serikali.

### 4.7.3 Mikakati

Mikakati ifuatayo itatekelezwa ili kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa hapa nchini zinanunulika katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Mikakati

hiyo ni:-

(i) Kuweka utaratibu wa upendeleo wa makusudi kwa wananchi katika utoaji wa tenda na zabuni.

(ii) Kuanzisha Kituo cha Uendelezaji wa Masoko kitakachoshughulikia kwa karibu utafiti wa masoko ya ndani na nje ya nchi, kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko na bei kwa wakati.

(iii) Kutumia taasisi za sekta binafsi na vyama vya biashara katika sekta mbalimbali kutoa taarifa za masoko.

(iv) Kutumia ubia na makampuni ya nje kwa makusudi ya kujipenyeza katika masoko ambayo tayari makampuni hayo yameshapata au wanayoweza kupata kwa kutumia uzoefu walio nao.

(v) Kutekeleza mikakati iliyobainishwa katika Mkakati wa Mauzo ya Nje ikiwa ni pamoja na Maeneo Maalum ya Mauzo ya Nje na Maeneo Maalum ya Kiuchumi pale itakapoonekena inafaa.

(vi) Kutumia taratibu za WTO ambazo zinaruhusu nchi maskini kulinda shughuli za kiuchumi za wananchi (anti-dumping).

(vii) Kutenga maeneo maalum kwa kila sekta kwa ajili ya shughuli za kiuchumi zitakazofanywa na wananchi.

## 4.8 USHIRIKA

### 4.8.1 Hoja

(i) Ushirika ni chimbuko la kujenga nguvu ya wananchi kuwa na sauti ya pamoja katika kufanya shughuli zozote zile. Katika mazingira ya uchumi wa soko huru wanaushirika wanahitaji vyama vilivyoundwa katika umoja kwa lengo la kuunganisha nguvu za raslimali zao katika kuendesha shughuli zao za biashara kwa ufanisi ili waweze kuhimili ushindani wa wafanyabiashara wengine katika soko.

(ii) Vyama vya Ushirika ni chombo cha kuwawezesha wananchi kiuchumi wakiwemo wakulima, wafugaji, wafanyabiashara, wenye viwanda, wachimba madini na wengineo ambao vinginevyo wasingeweza kushinda kwenye soko kama wafanyabiashara binafsi. Katika

kuimarisha na kuendeleza ushirika nchini, bado kuna mapungufu mengi yakiwemo; muundo usiokidhi mahitaji ya ushirika, kiwango kidogo cha elimu ya ushirika, uhaba wa mitaji, wanachama kutomiliki vyama vyao, wigo mdogo, uwezo mdogo wa kushindana kwenye soko huru, uongozi mbaya, wizi, ubadhirifu na hujuma.

### 4.8.2 Tamko la Sera

Serikali itaimarisha na kuendeleza ushirika nchini.

### 4.8.3 Mikakati

Ili kujenga ushirika imara, mikakati ifuatayo itatekelezwa:-

(i) Kuimarisha Vyama vya Ushirika vya Msingi na kuwawezesha wanachama kumiliki vyama vyao;

(ii) Kuongeza mitaji katika Vyama vya Ushirika;

(iii) Kuboresha uongozi, kudhibiti wizi, ubadhirifu na hujuma;

(iv) kuboresha muundo wa Ushirika;

(v) Kuimarisha Taasisi za Serikali zinazohusika na maendeleo ya ushirika;

(vi) Kuimarisha elimu na mafunzo ya ushirika kwa wanachama, viongozi na watendaji;

(vii) Kuongeza uwezo wa Vyama vya Ushirika wa kushindana ndani ya soko huru;

(viii) Kupanua wigo wa Ushirika;

(ix) Kuimarisha mfumo wa taarifa na takwimu za masoko na bei;

(x) Kuendelea kurekebisha Sheria ya Ushirika.

## 4.9 ARDHI

### 4.9.1 Hoja

Ardhi haijatumika kikamilifu katika kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za uchumi.

### 4.9.2 Tamko la Sera

Serikali itatumia ardhi kama njia muhimu ya kuwawezesha wananchi wake kushiriki kikamilifu kiuchumi. Lengo ni kusaidia wananchi watumie ardhi waliyo nayo ama kwa kujipatia hisa katika shughuli za uwekezaji huo au pato lenye kuwanufaisha kushiriki kikamilifu katika shughuli zingine za kiuchumi.

### 4.9.3 Mikakati

Mikakati ifuatayo itatumika kuhakikisha kwamba ardhi inatumika kama njia ya kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

(i) Kujenga miundombinu katika sehemu zenye rutuba na uwezo wa kuhimili kilimo ili ziweze kutumiwa na wananchi, hasa ambao sasa hawana ardhi, kuzalisha mali kikamilifu.

(ii) Kutoa ardhi kwa wawekezaji wakubwa kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Pale ambapo itabidi Wananchi wahamishwe ili kuwapisha wawekezaji wakubwa, Serikali itawasaidia utaalam wa kuingia katika makubaliano muafaka na wawekezaji kwa nia ya kuwanufaisha.

(iii) Kupima maeneo na kuweka miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kilimo, ufugaji, biashara na shughuli nyingine ndogo za kiuchumi.

(iv) Kuhakikisha kwamba ardhi inatumika kuwawezesha wananchi kupata mikopo.

## 5.0 MFUMO WA USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA SERA YA UWEZESHAJI

Mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi utazingatia mambo yafuatayo:-

(i) Ili kutekeleza mipango ya uwezeshaji katika sekta mbalimbali, ipo haja ya kuwa na mfumo wa usimamizi utakaogusa sekta zote za uchumi. Mfumo huo utawezesha kubuni, kupanga, kuratibu na kufuatilia maamuzi mbalimbali ya uwezeshaji wa wananchi.

(ii) Mfumo wa utekelezaji ni ule unaotoa mgawanyo mzuri wa kazi na ufafanuzi wa wajibu na majukumu ya wahusika wote katika ngazi mbalimbali.

(iii) Serikali itaweka mazingira yatakayozingatia kwamba, Sera ya Uwezeshaji itatekelezwa kwa kuzingatia misingi ya ushirikishwaji wa wadau wote

na itaunda taasisi maalum na mifuko itakayoongoza uendeshaji, usimamizi na utekelezaji wake. Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

**a) Baraza la Taifa la Uwezeshaji**

Baraza la Taifa la Uwezeshaji (National Economic Empowerment Council) kitakuwa chombo cha juu kitaifa kitakachokuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Chombo hicho kitaanzishwa chini ya Sheria ya Uwezeshaji ili kusimamia, kufuatilia na kuratibu shughuli zote za Uwezeshaji.

**b) Wakala wa Dhamana ya Mikopo**

Ili kuwawezesha wananchi kupata mitaji na dhamana kwa ajili ya miradi wanayoanzisha wao wenyewe au ile ya ubia na wageni, Serikali itaanzisha Wakala wa Dhamana ya Mikopo (Tanzania Credit Guarantee Agency) ambayo itashughulikia suala hilo. Taasisi hiyo itakuwa na kazi ya kutathmini miradi ya wananchi na pale inaporidhika, kutoa, dhamana ili wananchi waweze kukopeshwa na mabenki ya ndani na ya kimataifa, au kutoa mitaji kwa wananchi watakaoanzisha makampuni ya ubia na wawekezaji wa nje. Taasisi hiyo haitatoa mikopo ya moja kwa moja. Pale ambapo mfuko huo utakuwa umetoa dhamana, hisa za wananchi zitabakia mikononi mwa taasisi hiyo hadi hapo mkopo utakapokuwa umerejeshwa.

**c) Wakala wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

Ili kuwawezesha wananchi kujenga uwezo katika shughuli za kubuni na kusimamia utekelezaji wa miradi, pamoja na uendeshaji wa miradi inapokamilika, Serikali itaimarisha SIDO ili iweze kutekeleza jukumu hilo. Taasisi hiyo itashughulikia masuala yote yanayohusu maarifa ya kiufundi katika utekelezaji wa miradi, ubora wa bidhaa na masoko, ikiwa ni pamoja na ile miradi ambayo SIDO yenyewe itakuwa ikiisanifu na kuwapatia wananchi. SIDO itabadilishwa kuwa wakala wa kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo na za kati.

**d) Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali**

Ili kuongeza ujuzi kwa wananchi, hasa katika maarifa ya kiufundi, masoko na maendeleo ya biashara, Serikali itaanzisha Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali (Entrepreneur Development Institute (EDI) ambayo itasimamia masuala yote ya kuwawezesha wananchi kwa njia

ya kuwaongezea ujuzi. Hata hivyo, Taasisi hiyo haitatoa mafunzo moja kwa moja, bali itaandaa mitaala ambayo vyuo mbalimbali nchini vitatumia kuelimisha wananchi. Taasisi hiyo itaanzishwa chini ya chuo kimojawapo cha elimu ya juu kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo Kikuu cha Mzumbe au Chuo cha Biashara cha Dar es Salaam (CBE).

### e) Kituo Cha Uendelezaji wa Masoko

Katika jitihada za kukuza masoko ya ndani na nje ya nchi, Serikali itaunda Kituo cha Uendelezaji wa Masoko (Marketing Development Centre (MDC). Chombo hicho kitashughulikia kwa karibu utafiti wa masoko ndani na nje ya nchi, kukusanya, kuchambua kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko na bei kwa wakati.

### f) Benki ya Maendeleo ya Kilimo

Serikali itaanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo (Agricultural Finance Bank (AFB) ili kuendeleza shughuli za kilimo.

### g) Uanzishwaji wa Mifuko Mbalimbali

(i) Serikali itatumia mifuko mbalimbali itakayowezesha utekelezaji wa dhana nzima ya uwezeshaji wa wananchi. Mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi (Mwananchi Empowerment Fund), Mfuko wa Dhamana ya Mikopo, (Credit Guarantee Fund), Mfuko wa Amana ya Ubinafsishaji, (Privatization Trust) na Mfuko wa Umeme Vijijini, (Rural Electrification Fund).

(ii) Inatarajiwa kwamba mifuko hiyo itakayoanzishwa kwa muda muafaka baada ya kufanya utafiti wa kina, itawezesha utekelezaji wa masuala ya uwezeshaji bila kuhusisha Serikali moja kwa moja ingawa Serikali nayo itachangia katika mifuko hii. Mifuko hiyo itasimamiwa na mabenki yatakayoteuliwa na Serikali.